# JARIDA
## la Mtandaoni la NSSF

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

### NSSF YASHIRIKI MAONESHO YA 7 YA TEKNOLOJIA YA MADINI KWA MAFANIKIO




**NSSF**

Simu Bure
0800116773

@NssfTanzania

# RAIS MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN AKABIDHI TUZO KWA NSSF YA USIMAMIZI NA URATIBU WA HIFADHI YA JAMII KWA SEKTA BINAFSI NCHINI




Geita. Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umeshinda tuzo ya Usimamizi na Uratibu wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi nchini, wakati wa kilele cha Maonesho ya Saba ya Kitaifa ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika kwenye uwanja wa EPZ Bombambili, mkoani Geita. Tuzo hiyo imetolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, na kupokelewa na Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Bw. Masha Mshomba wakati wa ufungaji wa maonesho hayo.

Aidha, NSSF imeshinda tuzo ya mshindi wa kwanza katika kundi la Hifadhi ya Jamii na Huduma za Bima zilizotolewa Oktoba 12, 2024 na Mhe. Anthony Mavunde, Waziri wa Madini, wakati wa maonesho hayo.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa tuzo hiyo, Bw. Mshomba amesema utoaji wa huduma kidijitali umekuwa nyenzo muhimu katika kuhakikisha huduma za NSSF zinawafikia wanachama popote walipo, ikiwemo kufungua madai ya kuomba mafao mbalimbali.

Bw. Mshomba amewataka waajiri wa sekta binafsi kuhakikisha wanasajili wafanyakazi wao NSSF pamoja na kuwasilisha michango kwa wakati, kwani hilo ni takwa la sheria na vilevile kuwezesha Mfuko kuendelea kukua na kutoa huduma bora.

Aidha, Bw. Mshomba ametoa rai kwa watu waliojiajiri wenyewe katika sekta isiyo rasmi wakiwemo wachimbaji wadogo wa madini, mama lishe, baba lishe, boda boda, wavuvi, wakulima, wafugaji na wajasiriamali mbalimbali kujiunga na kuchangia NSSF kwa sababu ndiyo njia sahihi ya kupunguza umasikini wa kipato na kujikinga dhidi ya majanga mbalimbali.

Naye, Bw. Omary Mziya, Mkurugenzi wa Uendeshaji, amesema Mfuko utaendelea kutoa huduma bora kwa wanachama kupitia mifumo ya TEHAMA ambapo hivi sasa wanachama wanaweza kufungua madai yao kwa njia ya kidijitali bila ya kulazimika kufika katika ofisi za NSSF.

**"Utoaji wa huduma kidijitali umekuwa nyenzo muhimu katika kuhakikisha huduma za NSSF zinawafikia wanachama popote walipo, ikiwemo kufungua madai ya kuomba mafao mbalimbali"**

Kwa upande wake, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Bi. Lulu Mengele amesema kupitia maonesho hayo Mfuko ulifikisha elimu ya hifadhi ya jamii kwa makundi mbalimbali yakiwemo ya wachimbaji wadogo wa madini pamoja na wajasiriamali zaidi 1500 Wilayani Bukombe.

"Maonesho ya madini yalikuwa fursa kwa NSSF kufikisha elimu ya hifadhi ya jamii, kuandikisha wanachama wapya kutoka sekta isiyo rasmi, tutoa elimu kuhusu huduma za kidijitali pamoja na fursa za nyumba na viwanja," amesema Bi. Lulu.

Awali, Meneja wa NSSF Mkoa wa Geita, Bi. Winniel Lusingu amesema katika mwaka wa fedha 2024/25, Ofisi ya Mkoa huo imeweka lengo la kukisanya shilingi bilioni 104 na kuwa mwaka wa fedha uliomalizika walikusanya shilingi bilioni 64. Ameshukuru ushirikiano mkubwa wanaopata kutoka kwa uongozi wa Mkoa huo, Waajiri, Menejimenti na Wafanyakazi wote wa NSSF.

# NSSF YATUMIA FURSA YA MAONESHO YA MADINI GEITA KUTOA ELIMU YA HIFADHI YA JAMII

**Na MWANDISHI WETU**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ulitumia Maonesho ya Saba ya Teknolojia ya Madini kutoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi ikiwemo Sekta ya Madini.

Akizungumza na mamia ya wananchi waliojitokeza katika ufunguzi wa maonesho hayo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Biteko Biteko alisema maonesho yametoa fursa ya wananchi kupata elimu kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu uwekezaji kwenye sekta ya madini.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara wa madini kutumia mazingira rafiki yaliyowekwa na Serikali ya awamu ya sita katika kuboresha mazingira ya uwekezaji ili wafanye biashara zao kwa uhuru na kukuza uchumi.

Naye, Waziri wa Madini, Mhe. Anthony Mavunde alisema mchango wa sekta ya madini unaendelea kukua siku hadi siku na kuwa wanatarajia hadi kufikia mwakani, sekta ya madini iwe inachangia katika pato la Taifa kwa asilimia kumi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhe. Martine Shigela alisema maonesho ya mwaka huu yameshirikisha zaidi ya washiriki 800 na yamechangia mafanikio ya mkoa huo.

Awali, akizungumza mbele ya Naibu Waziri Mkuu, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Bw. Masha Mshomba, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma, Bi. Lulu Mengele alisema NSSF inashiriki maonesho hayo kwa malengo ambapo katika mwaka wa fedha 2023/24, Mfuko kupitia Ofisi ya Mkoa wa Geita iliweza kukusanya shilingi bilioni 64 na kuwa asilimia 80 ya fedha hizo zilikusanywa kwenye makampuni mbalimbali ya madini.

Bi. Mengele alisema sekta ya madini ni wadau muhimu wa NSSF wakiwemo wachimbaji wadogo, wa kati na wakubwa ambao wote ni wanachama wa Mfuko na kuwa wamekuwa wakikusanya kiasi kikubwa cha fedha kutoka kwenye sekta ya madini.

Alisema NSSF imeendelea kuboresha huduma kupitia mifumo ya TEHAMA, ambapo kwa sasa wanachama wa NSSF wanaweza kufungua madai yao kidijitali huko huko waliko lengo ni kuondoa kero za wanachama na kusogeza huduma hukohuko waliko. Pia waajiri wanalipia michango ya wanachama wao wakiwa Ofisini bila ya kufika katika ofisi za NSSF.

Bi. Lulu alisema kupitia mifumo imechagiza mafanikio ya NSSF ambapo thamani imekua na kufikia trilioni 8.6. "Tunakushukuru sana mgeni rasmi hii ni kazi kubwa ya nyie viongozi mnayoifanya kutuongoza," amesema Bi.Lulu Mengele











# HABARI PICHA

## USHIRIKI WA NSSF KATIKA MAONESHO YA 7 YA MADINI






# WAAJIRI SEKTA BINAFSI WASILISHENI MICHANGO YA WAFANYAKAZI WENU NSSF

**Na MWANDISHI WETU**

Mgeni rasmi wa siku ya mifuko ya hifadhi ya jamii na bima, Bw. Simon Shayo ambaye pia ni Makamu wa Rais wa GGM, akizungumza na washiriki wa kongamano hilo, ambapo alisisitiza umuhimu wa waajiri wa sekta binafsi kuwasilisha michango ya wafanyakazi wao kwenye Mfuko wa NSSF pamoja na wajasiriamali kujiunga na kuchangia ili waweze kunufaika na mafao yanayotolewa na Mfuko.













# NSSF YASHIRIKI BUKOMBE RUNNERS

**Na MWANDISHI WETU**

Bukombe. Baadhi ya Wafanyakazi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) wakiongozwa na Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma, Bi. Lulu Mengele wameshiriki mbio fupi za kilomita 5 Bukombe Mkoani Geita, zinazojulikana kama 'Bukombe Runners Club' ambapo mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko.

NSSF inatumia matamasha kama hayo kufikisha elimu ya hifadhi ya jamii lakini pia ni kuunga mkono juhudi za Serikali katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza.

Aidha, NSSF ilitumia fursa hiyo kufikisha elimu ya hifadhi ya Jamii kwa wajasiriamali zaidi ya 1500 wanaofanya shughuli mbalimbali za kiuchumi ambao walielezwa umuhimu wa kujiunga na kujiwekea akiba ili waweze kunufaika na mafao yanayotolewa na NSSF














Baadhi ya wajasiriamali wanaofanya shughuli mbalimbali wakifuatilia wasilisho kutoka kwa watumishi wa NSSF kuhusu umuhimu wa hifadhi ya jamii

# HABARI PICHA

## MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA USHIRIKI WA NSSF MAONESHO YA 7 YA MADINI












Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF),
Jengo la Benjamin William Mkapa, Mtaa wa Azikiwe
S.L.P 1322, Dar es Salaam, Tanzania

Simu Bure: 0800116773,
Barua pepe: customercare@nssf.go.tz
Tovuti: www.nssf.go.tz

@NssfTanzania